

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS-TAMISEMI**



**Namba za simu:**

**Shule ya Sekondari Songe**

**Mkuu wa shule 0782012081/0768495193**

**S. L. P 1440**

**Makamu Mkuu wa Shule 0752617608**

**Musoma**

**Matron Na: 0769773770**

**Matron Na: 0755802187**

**Tarehe: 06/05/2024**

**Ndugu Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi.....**

.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SONGE,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA, MKOA WA MARA MWAKA 2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024, na atasoma tahasusi (combination) aliyopangiwa na wizara. Shule hii ipo umbali wa Km (7) Mashariki mwa mji wa Musoma, Mita 400 kutoka barabara kuu iendayo Mwanza. Usafiri wa daladala kutoka mjini au stendi ya mabasi ya Mikoani Bweri unapatikana katika vituo vya stendi za daladala za mjini na Bweri kwa nauli ya shilingi 500/. Pia unaweza kukodi bajaji au pikipiki (bodaboda) kutoka stendi ya bweri hadi Songe Shuleni kwa nauli ya shilingi 2,000/= au 3,000/
2. Muhula wa masomo utanza julai 2024 kwa hiyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku za kazi kuanzia tarehe.....na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/7/2024 na muda wa kupokelewa ni kuanzia saa 2:00asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

- 2. Mambo ya kuzingatia:-

- 2.1 Sare ya shule

- Sare ya shule hii ni sketi ndefu mbili (2) za rangi ya bluu bahari (Kitambaa kizito) zenye marinda ya kawaida zinazofika kisiginoni (na sio rinda box). Kwa mzazi anayependa kununua shuleni **zinapatikana kwa shs 22,000/= kwa sketi moja.**
    - Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi.
    - Kwa waislamu kijuba cha rangi nyeupe na nusu kanzu isiyobana nyeupe.
    - Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi ( **visiwe vya Buti**)
    - Sare ya michezo ni Bukta na T-shirt za rangi ya dark blue au bluu na raba nyeupe
    - Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na alama yoyote
    - Sweta ya rangi ya **Blue** yenye alama ya **V** shingoni. Kwa mzazi anayependa kununua shuleni inapatikana kwa Shs. 10,000/=
  - Nguo za kushindia (shamba dress) ni gauni mbili (2) za rangi ya **Premium Vector Blue** (kitambaa kizito) Mshono wake ni solo ndefu inayo fika kwenye kisigino, yenye mikono mifupi na shingo yenye **V** kifuani. Kwa waislamu inakuwa ya mikono mirefu na kijuba kifanane na Rangi ya Shamba Dress. (Kwa mzazi anayependa kununua shuleni Gauni ni 2@ Tsh 24,000/= jumla inakuwa Tsh 48,000/=)
  - Huruhusiwi kusuka unatakiwa kuwa na nywele fupi
  - Mapambo ya aina yoyote hayaruhusiwi (mfano: kupaka rangi ,kuvaa, hereni, bangiri nk.)
  - Nguo za nyumbani ,manukato (perfumes),vinywaji na vyakula vya aina yoyote haviruhusiwi kabisa.

## 2:2 Michango ya shule

- Mchango wa uendeshaji wa shule .....65,000/=
  - Tahadhari.....5,000/=
  - Nembo.....5,000/=
  - Kitambulisho cha shule .....5,000/=
- JUMLA.....80,000/=

**Nb : Fedha zote zitalipwa kwenye akaunti ya shule 30310012473, Jina Songe Sekondari, Benki ya NMB, andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip**

## 2:3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- Ream ya karatasi moja (**A4 BOUBLE A**) kwa muhula au mbili kwa mwaka.
- Vitabu vya masomo ya tahasusi (**Orodha imeambatanishwa**)
- Sanduku la bati kwa ajiri ya kutunzia vitu vyake
- Tochi kwa tahadhari usiku umeme ukikatika
- Madaftari makubwa (Counterbooks Q4) yasiyopungua saba na madaftari madogo saizi ya kati saba kwa ajili ya mazoezi.
- Kalamu, Rula na ufuto
- Scientific calculator na Mathematical Set kwa watakaosoma somo la Jiografia
- Godoro la Sponge la futi mbili na nusu kwa 6 na mto
- Mashuka mawili rangi ya pinki, Foronya 1, na chandarua cha rangi nyeupe cha mviringo.
- Kamusi (Watakaosoma somo la Kiswahili) na English dictionary kwa wote
- Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli, Kijiko, Kikombe na Kidumu cha kutunzia maji ya kunywa)

- Fedha ya matumizi yake binafsi
- Ndoo ndogo moja na kubwa moja na kikombe kikubwa cha kuogea
- Nguo za ndani za kutosha zisizo pungua sita,aje na vesti nyeupe(spider)
- Mwanafunzi aje na bima ya afya ya NHIF na kama hana aweke Tsh 50,400/= kwenye akaunti ya shule ili akatiwe bima
- **Vifaa vya usafi :**

#### **HGK**

- Ufagio wa nje (Chelewa ya mafungu na si ile yenye mti)
- Fyekeo
- Jembe lenye Mpini
- Brashi ndogo ya chooni(Toilet brush)

#### **HGL**

- Ufagio wa nje(Chelewa ya mafungu na si ile yenye mti)
- Hard broom
- Fyekeo
- Dawa ya Chooni lita (5) aina ya dawa ni Dexi

#### **HKL**

- Ufagio wa nje(Chelewa ya mafungu na si ile yenye mti)
- Jembe lenye mpini
- Fyekeo.
- Squizer za kukaushia maji.

- SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafanuliwa na maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamiya na;-

### 3.1 Sheria na kamuni za Shule

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima,
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)
- Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa/sale ya shule wakati wa vipindi na shamba dress baada ya vipindi.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za shule.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vifaa nya ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

### **MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na haruhusiwi kumpa mtumishi yeyote simu amtunzie.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala katika bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**


**kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bwani ambalo hukupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule. (Msiba au Ugonjwa)**
  - **Kwa kuwa mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni, mzazi unatakiwa kutumia simu zenye namba zilizo rodheshwa hapo juu kwa mawasiliano pamoja na kutuma fedha kwa ajili ya mwanao. Unapotuma pesa tuma na ujumbe mfupi ukitaja jina la mwanafunzi na kiasi ulichotuma.**
- 
- **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**
    - Wizi
    - Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
    - Kugoma au kuhamasisha mgomo
    - Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
    - Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule
    - Kusuka/Kufuga nywele ndefu au kunyoa mtindo usiokubalika
    - Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
    - Uvutaji wa sigara
    - Uasherati, uhusiano wa jinsia moja au kuolewa
    - Kupata ujauzito au kutoa mimba
    - Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
    - Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni uwapo shuleni
    - Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
    - Kudharau Bendera ya Taifa
    - Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
    - Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

- Viambatanisho na Fomu Muhimu
  - Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali
  - Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
  - Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
  - Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu (Picha zibandikwe kwenye Jedwali husika
  - Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu awe na vitu vifuatavyo;
    - Kivuli cha cheti cha kuzaliwa kinachotolewa na Serikali (**Birth Certificate**)
    - Kivuli cha hati ya matokeo ya kidato cha Nne (**Results Slip**)
- Tafadhari soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## **KARIBU SANA SONGE SEKONDARI**

**Mkuu wa Shule**

 P. E. ADMISTRESS  
 SONGE SEC. SCHOO.  
 P. O. BOX 1440  
 NUSOMA

**ROSEMARY B. JOHN**

**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia a mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KWA NAMBA ZILIZO WEKWA KATIKA FOMU HII.**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII  
WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye Sel Form)  
.....
2. Anwani ya nyumbani  
.....
3. Tarehe ya kuzaliwa .....
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji.....  
Kata.....Tarafa.....  
Wilaya.....Mkoa.....
5. Mahali unapoishi kwa sasa .....
6. Shule ya Sekondari  
ulikutoka..... Anwani  
**(Muhimu sana)** .....
7. Dini/Dhehebu.....
8. Kabila.....
9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania).....
10. Baba na Mama wanaishi au hawaishi? (a) Baba ..... (b) Mama .....
11. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu

SN	JINA	PICHA	UHUSIANO	KAZI	NAMBA YA SIMU
1					
2					
3					



4					
---	--	--	--	--	--

kwa masuala ya shule:

**12. Ahadi ya utii:**

(a) Mimi (Mwanafunzi).....nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

.....  
Sahihi ya Mwanafunzi

.....  
Tarehe

(b) Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi).....  
ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi .....  
nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Songe ambako binti yangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoielezwa na kumtimizia mahitaji yake na kulipa ada ya shule na michango mingine yote. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

.....  
Sahihi ya Mzazi/Mlezi

.....  
Tarehe

**SONGE SECONDARY SCHOOL  
MEDICAL EXAMINATION FORM**

**SONGE SECONDARY SCHOOL,  
P.O. Box 1440,  
MUSOMA.  
DATE.....**

**To Medical Officer,**  
.....  
.....

**Ref.....  
(NAME OF STUDENT)**

Please examine the above named Student as per Medical examination form below,

*R. Boti*

**HEADMISTRESS  
MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by Government Medical Officer)

Full Name.....

Age.....Height..... (cm)      Weight..... (Kg)

- Blood count (Red and White).....
- Stool Examination.....
- Urinary analysis.....
- STD<sub>s</sub> and other V.D.....
- T.B and Leprosy test.....
- Eye test.....
- Ear test.....
- Chest .....
- Abdominal test.....
- Blood Group (**Very Crucial**).....
- Spleen.....
- Pregnancy test.....
- Bilharzias .....
- Asthma.....
- Skin diseases.....

16. Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g. Sick cell)

.....

I have examined the above named student and I certify that she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

Signature.....Date.....

Station.....

Designation and Official Stamp.....

**ORODHA YA VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI MWANAFUNZI  
ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO**

• **GENERAL STUDIES:**

- Mwajabu, M (2016) Comprehensive Book for Advanced Level Secondary School
- Nyambari, N & Bukagile, R (2010), Contemporary Approach for Advanced Level General Studies Form 5 & 6
- TIE (2022) General Studies for Advanced Secondary School.

• **HISTORY:** TIE (2022) History for Advanced secondary school student's Book Form Five.

- Oxford (2011) Advanced Learners History Form 5 & 6

• **GEOGRAPHY:**

- Zist, K (2015) ,Geography Paper Two, Human and Economic Geography
- Zist, K (2016), Physical Geography Paper One
- TIE (2022) Practical Geography For Advanced Secondary School.

• **KISWAHILI:**

- Oxford University Press (2012) Kiswahili Kidato cha Tano na Sita
- Nyangwine Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 Kidato cha 5 na 6
- J .A. Masebo (2006) Nadharia ya Fasihi Kiswahili 2 Kidato cha 5 na Sita
- Tahakiki za vitabu
- Riwaya-Vuta n kuvute,kufikirika,mfadhili,usiku utakapokwisha
- Tamthiliya-nguzo mama,kivuli kinaishi,kwenye ukingo wat him,morani
- Ushairi-kimbunga,chungu tamu,funigate ya uhuru

• **ENGLISH:**

- English Paper One. Ashel, N (2010): Advanced Level English A practical Approach
- Paper Two. Ashel N (2011) Advanced Level Literature An Essential Guide
- Paper Two.Mgonja (2019)Analytical Analysis Advenced Literature

